



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

MKUTANO WA KUKUSANYA MAONI KUHUSU VIWANGO VYA NAULI ZA ABIRIA KWA TRENI YA SGR KWA MIKOA YA DAR ES SALAAM – MOROGORO-DODOMA-HADI BAH

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imepokea maombi kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuhusu nauli za abiria kwa treni ya njia ya Reli ya Kisasa – ‘Standard Gauge Railway’ (SGR) zitakavyotumika kwa huduma ya usafiri wa treni za abiria.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria Na. 3 ya LATRA, 2019 Mamlaka inapaswa kukusanya maoni ya wadau kabla ya kufikia uamuzi wa kuridhia viwango vya nauli kwa huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka ikiwemo nauli za treni.

Katika kulitekeleza hilo, Mamlaka imeandaa mkutano wa kupokea maoni ya wadau wa usafirishaji, ikiwa ni pamoja na watoa huduma, watumiaji wa huduma na wananchi kwa ujumla. Mkutano utafanyika tarehe 19 Disemba 2022 jijini Dar es salaam katika Ukumbi wa Anatorglo.

Nauli zinazopendekezwa na TRC ni Kama ifatavyo:

Mapendekezo ya Nauli za Awali za Kuanza kutoa Huduma Dar es salaam kwenda vituo Mbalimbali-Viwango ni kwa TSHS kwa Abiria						
Na	Kutoka	Kwenda	Daraja Kawaida		Daraja la Kati	
			Mkubwa	Mtoto miaka (4- 12)	Mkubwa	Mtoto miaka (4- 12)
1	Dsm	Soga	9,494	4,747	11,392	5,696
2		Ruvu	14,394	7,197	17,272	8,636
3		Ngerengere	19,494	9,747	23,392	11,696
4		Morogoro	24,794	12,397	29,752	14,876
5		Mkata	30,194	15,097	36,232	18,116
6		Kilosa	35,694	17,847	42,832	21,416
7		Kidete	41,394	20,697	49,672	24,836
8		Gulwe	47,294	23,647	56,752	28,376
9		Igandu	53,294	26,647	63,952	31,976
10		Dodoma	59,494	29,747	71,392	35,696
11		Bahi	65,894	32,947	79,072	39,536

**Mapendekezo ya Nauli za Awali za Kuanza kutoa Huduma Kituo kwa Kituo - Viwango ni
kwa TSHS kwa Abiria**

Na	Kutoka	Kwenda	Daraja Kawaida		Daraja la Kati	
			Mkubwa	Mtoto miaka (4- 12)	Mkubwa	Mtoto miaka (4- 12)
1	Dsm	Pugu	4,694	2,347	5,632	2,816
2	Pugu	Soga	4,800	2,400	5,760	2,880
3	Soga	Ruvu	4,900	2,450	5,880	2,940
4	Ruvu	Ngerengere	5,100	2,550	6,120	3,060
5	Ngerengere	Morogoro	5,300	2,650	6,360	3,180
6	Morogoro	Mkata	5,400	2,700	6,480	3,240
7	Mkata	Kilosa	5,500	2,750	6,600	3,300
8	Kilosa	Kidete	5,700	2,850	6,840	3,420
9	Kidete	Gulwe	5,900	2,950	7,080	3,540
10	Gulwe	Igandu	6,000	3,000	7,200	3,600
11	Igandu	Dodoma	6,200	3,100	7,440	3,720
12	Dodoma	Bahi	6,400	3,200	7,680	3,840

Kutokana na umuhimu wa mkutano huo, LATRA inawaalika wadau wa sekta ya reli na wananchi kwa ujumla kushiriki katika mkutano huo wa kukusanya maoni ya wadau.

Vilevile, wadau wanaweza kuwasilisha maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu kwa maandishi kupitia LATRA Makao Makuu, Mtaa wa Tambuka Reli, Dodoma au ofisi za LATRA zilizopo Makao Makuu ya kila mkoa Tanzania Bara kabla ya tarehe 3 Januari 2023.

Aidha, maoni ya wadau yanaweza kutumwa kwa barua pepe kupitia anuani hizi: info@latra.go.tz na dq@latra.go.tz

**Imetolewa na:
Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano – LATRA
06 Disemba, 2022**